**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA**
**SHULE YA SEKONDARI MADANGWA**
**S.L.P 630 LINDI**

---

**12 Disemba, 2020**

**Kumb. Na. MAD/S2465/JI/F1/2021**

**Mzazi/Mlezi wa: ________________________________________**
**Shule ya Msingi: ________________________________________**

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA MADANGWA KWA MWAKA WA MASOMO WA 2021**

1. Jumuiya ya Madangwa Sekondari ina furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza katika shule hii ya Sekondari kwa mwaka wa masomo 2021. Nampongeza sana kwani hii ni nafasi adhimu sana katika kuyajenga maisha yake.

2. Ni imani yangu kuwa ataitumia fursa hii kikamilifu yaani kwa nguvu zote, akili zote na jitihada zote ili aweze kufikia malengo yake ya baadae na ya Taifa kwa ujumla. Mafanikio ya kielimu siku zote huletwa na **Nidhamu, Kujiamini (Kuwa naweza), Kujituma, Kutokata tamaa, Kuvumilia, Usikivu, Kujielewa (Kuwa na malengo) na Utayari.** Pia **Ushirikiano wa Mzazi au Mlezi** katika utekelezaji wa malengo ya kielimu. Mzazi tusaidiane katika kuyasisitiza haya mara kwa mara.

3. Shule ya Sekondari Madangwa ni shule ya Kata ya Sudi inayopatikana kijiji cha Madangwa. Shule ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko (Wavulana na Wasichana). Mwanafunzi atalazimika kuja shule akitokea nyumbani. Aidha, napenda kukujulisha kuwa shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** siku ya **Jumatatu** na hivyo mtoto wako anatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe na siku hiyo **saa 1:00 Asubuhi**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**. Baada ya hapo vyombo husika vitafanya msako kwa wasioripoti na kuwashughulikia kisheria.

4. Masomo yanayofundishwa hapa shuleni ni **Civics**, **History**, **Geography**, **Kiswahili**, **English Language**, **Physics**, **Chemistry**, **Biology**, **Basic Mathematics** na **Literature in English (Kuanzia Kidato cha Tatu)**. Masomo yote, isipokuwa **Kiswahili** yanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza hivyo suala la kujifunza, kukielewa na kukitumia Kiingereza ni la muhimu sana.

5. Pamoja na barua hii, nimeambatanisha fomu zifuatazo ili zisomwe na zijazwe kikamilifu na kuwasilishwa hapa shuleni siku ya kuripoti. Fomu zinazotakiwa kujazwa na kurudishwa shuleni ni Fomu namba 1 na Fomu namba 4. Fomu nyingine ni pamoja na;
   - Fomu Na. 1: Vipimo vya Afya,
   - Fomu Na. 2: Mahitaji Muhimu ya shule na Mwanafunzi,
   - Fomu Na. 3: Sheria, Kanuni na Taratibu za shule,
   - Fomu Na. 4: Kukiri utiifu (mwanafunzi na Mzazi/Mlezi).

**FRANCISCO ZEBEDAYO**
**KAIMU MKUU WA SHULE**

**Form No: 1**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MTAMA DISTRICT COUNCIL**
**MADANGWA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 630 LINDI**

---

**12th December, 2020**

**Ref. No: MAD/S2465/JI/F1/2021**

To The Medical Officer (District / Regional)
______________________________
______________________________
______________________________

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS______________________________________**

Please examine the above named pupil and give us a report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Pupils Full Name: ______________________________
2. Blood: ______________________________
3. Stool: ______________________________
4. T.B Test: ______________________________
5. Urine Examination:______________________________
6. Syphilis Examination: ______________________________
7. Eye Test: ______________________________
8. Chest Test: ______________________________
9. Ears Test: ______________________________
10. Spleen: ______________________________
11. Abdomen : ______________________________
12. Pregnancy (For Girls Only): ______________________________

Any additional information: e.g physical defects or impairment, infection, family diseases etc.
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

I certify that the above pupil is **SUITABLE/UNSUITABLE** for secondary school studies. If unsuitable give reasons.
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

Name of MEDICAL OFFICER: ______________________________

Signature of MEDICAL OFFICER: ______________________________

**Date**:______________________________ **Official Stamp** ______________________

**Form No: 2**

## MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

**SARE YA SHULE**

**(A) WAVULANA**

- Suruali mbili rangi ya "**Blue Bahari**" kitambaa kizito cha suti (Istima namba 1) mbele iwe na marinda mawili. Suruali lazima ifunike visigino vya viatu na isiwe "modo". **Mzazi simamia kwa umakini suala hili ili kuepusha usumbufu wa mtoto kurudishwa.**
- Mashati mawili meupe mikono mifupi ya kitambaa cha tetroni.
- Viatu vyeusi vya ngozi.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Bukta nyeusi na T-shirt nyeupe. Jezi rangi ya bluu juu na chini pamoja na raba kwa ajili ya michezo.

**(B) WASICHANA**

- Sketi mbili ndefu kuvuka magoti za rinda za kupanga za rangi ya "**Blue Bahari**", kitambaa kizito (Istima namba 1). **Mzazi simamia hili kwani ni marufuku kuvaa sketi fupi.**
- Nusu kanzu mbili nyeupe mikono mirefu (Kama mtoto atavaa hijab) au mashati mawili mikono mifupi kama hatovaa hijab. Kitambaa ni tetroni na shati liwe na kola shingoni.
- Hijab nyeupe sana (kwa wanaohitaji kuvaa) ya kujihifadhi lakini isiwe kibwaya.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Track suit rangi ya bluu, T-shirt rangi nyeupe na raba kwa ajili ya michezo.

**NB**: 'Wasichana **hawaruhusiwi** kusuka".

## MAHITAJI MUHIMU YA SHULE NA MWANAFUNZI

Kwa sababu za usafi binafsi wa mwanafunzi akiwa hapa shule na mazingira ya kujifunzia pamoja, usajili na uchukuaji mzuri wa masomo yake, mwanafunzi anapaswa kuwa na vifaa vifuatavyo:

- Daftari za kutosha 12 (ziwe counter book kuanzia Quire 2), kalamu za wino na risasi na mkebe (Mathematical set) 1.
- Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili au Kiswahili – Kiingereza.
- Ndoo moja ndogo (yenye mfuniko) na ufagio size ya kati wa kufagilia nje.
- Faili moja (hasa la plastic) kwa ajili ya kuhifadhia mitihani yake pamoja na majaribio mbalimbali.
- Chakula (Unga 6kg, Maharage 4kg, Sukari ½ kg, fedha Tsh. 5,000/=) kila mwezi kwa ajili ya mlo wa asubuhi na mchana.

**NB: Mahitaji yote hayo ni ya muhimu hivyo kila mzazi/mlezi ni budi kuyatimiza yote na kwa wakati**.

**Form No: 3**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA**
**SHULE YA SEKONDARI MADANGWA**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **sheria Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya kusimamia Elimu nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Katika kipindi chote utakachokuwa hapa shuleni, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

1. Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu Walimu, Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wasio walimu, Wageni, Wanafunzi wenzake na jamii yote ndani na nje ya shule.
2. Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu viongozi wa serikali ya wanafunzi (viranja) waliochaguliwa na wanafunzi wenzake ndani na nje ya shule.
3. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima.
4. Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi jioni (preparation).
5. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
6. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
7. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
8. Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo; na
9. Kutunza mali za shule.

### MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
e) Kupiga au kupigana.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito / Kupata mimba (Kwa wasichana) au kusababisha mimba (Kwa wavulana).
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu wengine.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi, na
m) Kuwa na simu ya mkononi au line ya simu katika eneo la shule.

**Form No: 4**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA**
**SHULE YA SEKONDARI MADANGWA**
**S.L.P 630 LINDI**

---

## HATI YA KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE

### (A) MWANAFUNZI

Mimi……………………………………………………………….ninakubali kuchukua nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari ya Madangwa. Ninaahidi kuwa nitatii sheria zote, kanuni na maelekezo yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule na kwamba nitajitahidi na kushirikiana na wana jumuiya wa Madangwa Sekondari katika shughuli zote za MASOMO, KAZI na MICHEZO katika kipindi chote cha uanafunzi wangu. Na kwamba kwenda kinyume na kiapo hiki ni kutoa nafasi kwa hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yangu.

| Jina la Mwanafunzi | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|
| ……………………………………………. | ……………………… | ……………………….. |

### (B) MZAZI / MLEZI

Mimi……………………………………………………………………………………………………ambaye ni Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi…………………………………………………………………nakubali mtoto wangu ajiunge na shule ya Sekondari Madangwa na kufuata taratibu zote zilizowekwa. Nakubali kuwa nitatoa mahitaji yote ya mwanafunzi yanayonihusu pamoja na kufuata maelekezo yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule kama inavyostahili. Nafahamu kuwa kutotekeleza majukumu hayo kutapelekea nichukuliwe hatua za kisheria.

Jina la Mzazi/Mlezi: ………………………………………………………………………………………………………

Kazi anayofanya …………………………………………………………………Simu …………………………………..

Kijiji/Mtaa ………………………………………………………………………Kata …………………………………..

Anuani ……………………………………………………......................Sahihi…………………………………..

Tarehe……………………………

### (C) MAJINA NA TAARIFA ZA VIONGOZI WAKE WA KIJIJI / KITONGOJI

1. Mwenyekiti wa kijiji:…………………………………………………...........Simu ……………………………

2. Mtendaji wa Kijiji: …………………………………………………………………..Simu ……………………………

3. Mwenyekiti wa Mtaa/Kitongoji: …………………………………………………Simu …………………………..